# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## MKOA WA MBEYA

# MPANGO MKAKATI WA KUENDELEZA SEKTA ZA KILIMO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2020 – 2025


**Imeandaliwa na:**

**Ofisi ya Mkuu wa Mkoa**
**S.L.P 754**
**MBEYA.**

**Simu:2504045/2502035**
**Nukushi:2504243/2500889**


**2020**

## YALIYOMO

**YALIYOMO** ..... **ii**
**ORODHA YA MAJEDWALI** ..... **iv**
**MAUMBO** ..... **v**
**VIFUPISHO** ..... **vi**
**KAULI YA MHESHIMIWA MKUU WA MKOA** ..... **vii**
**SHUKRANI** ..... **vii**
**DIBAJI** ..... **x**
**SURA YA KWANZA:UTANGULIZI** ..... **1**
1.1 Mahali ulipo Mkoa ..... 1
1.2 Eneo, Idadi ya Watu ..... 1
1.3 Pato la Mkoa ..... 1
1.4 Hali ya Ulinzi na Usalama ..... 1
1.5 Kanda za Uzalishaji ..... 2
1.5.1 Ukanda wa Juu ..... 2
1.5.2 Ukanda wa Kati ..... 2
1.5.3 Ukanda wa Chini ..... 2
**SURA YA PILI:UCHAMBUZI WA HALI HALISI NA WADAU** ..... **3**
2.0 Utangulizi ..... 3
2.1. Uchambuzi wa Wadau ..... 3
2.2. Uchambuzi wa Hali Halisi ..... 7
**SURA YA TATU:DIRA, DHIMA, MISINGI YA TAASISI NA MALENGO** ..... **9**
3.0 Utangulizi ..... 9
3.1. Dira ..... 9
3.3. Misingi ya Taasisi ..... 9
3.4.1. Lengo Kuu ..... 9
3.4.2. Malengo Mahususi ..... 9
**SURA YA NNE:MPANGO MKAKATI WA MKOA WA KUENDELEZA SZK MWAKA 2020 – 2025** ..... **10**
4.0 Utangulizi ..... 10
4.1 Sekta ya Kilimo 2015-2020 na Mpango Mkakati wa 2020-2025 ..... 11

4.1.1 Eneo la Kilimo ........ 11
4.1.2 Uzalishaji wa Mazao (2015-2020) ........ 11
4.1.3 Umwagiliaji ........ 12
4.1.4 Mazao ya Chakula ya Kipaumbele ........ 12
4.1.5 Mahitaji na Usalama wa Chakula ........ 13
4.1.6 Mazao ya Kimkakati ya Biashara ........ 13
4.1.7 Mkakati wa Mkoa katika kuongeza uzalishaji na tija (2020-2025) ........ 14
4.2 Sekta ya Mifugo 2015-2020 na Mpango Mkakati wa 2020-2025 ........ 16
4.2.1 Hali ya Uzalishaji wa Mifugo kwa kipindi cha 2015-2020 ........ 16
4.2.2 Miundombinu na Malisho ya Mifugo ........ 17
4.2.3 Magonjwa ya Mifugo ya Kimkakati ........ 17
4.2.4 Mkakati wa Kuongeza Uzalishaji na Tija (2020-2025) ........ 18
4.3 Sekta ya Uvuvi 2015-2020 na Mpango Mkakati wa 2020-2025 ........ 20
4.3.1 Hali ya Uzalishaji wa Sekta ya Uvuvi (2015-2020) ........ 20
4.3.2 Mkakati wa Kuongeza Uzalishaji na Tija (2020-2025) ........ 21
4.4 Sekta ya Ushirika ........ 21
4.4.1 Hali ya Ushirika katika Mkoa ........ 21
4.4.2 Huduma za Vyama vya Ushirika ........ 22
4.5 Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Ushirika 2020-2025 ........ 24
**SURA YA TANO:UFUATILIAJI NA TATHMINI ........ 25**
5.0 Utangulizi ........ 25
**SURA YA SITA:HITIMISHO ........ 26**

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali Na. 1:** Uchambuzi wa Wadau wa Sekta za Kilimo ........ 3

**Jedwali Na. 2:** Uchambuzi wa Hali Halisi Mkoa wa Mbeya ........ 7

**Jedwali Na. 3:** Eneo la Kilimo ........ 11

**Jedwali Na. 4:** Eneo (Ha) la Umwagiliaji ........ 12

**Jedwali Na. 5:** Uzalishaji wa Mazao ya Kipaumbele (2015 -2020) ........ 13

**Jedwali Na. 6:** Wastani wa Mahitaji ya Chakula/Mwaka/Tani (2015-2020) ........ 13

**Jedwali Na. 7:** Uzalishaji wa Mazao ya Kimkakati ya Kibiashara (2015 -2020) ........ 14

**Jedwali Na. 8:** Matarajio ya Tija kwa Mazao ya Kipaumbele ya Chakula ........ 15

**Jedwali Na. 9:** Matarajio ya Tija na Ubora kwa Mazao ya Kimkakati ya Biashara ........ 16

**Jedwali Na. 10:** Bei Elekezi ya Magonjwa 13 ya Mifugo ya Kimkakati ........ 17

**Jedwali Na. 11:** Idadi ya Vyama Vikuu / miradi wa Pamoja, SACCOS, na Vyama Vingine vya Ushirika ........ 21

## MAUMBO

**Umbo Na. 1:** Idadi ya Mifugo........................................................................ 17

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AMCOS | Agricultural Marketing Cooperatives Societies |
| ASDP | Agricultural Sector Development Programme |
| BPS | Bulk Procurement System |
| CBPP | Contagious Bovine Pleuropneumonia |
| CCPP | Contagious Caprine Pleuralpneumonia |
| DADPs | District Agricultural Development Plans |
| ECF | East Coast Fever |
| FMD | Foot and Mouth Disease |
| LATRA | Land Transport Regulatory Authority |
| MATI | Ministry of Agriculture Training Institute |
| NEMC | National Environmental Management Council |
| OSHA | Occupational Safety and Health Administration |
| PPR | Peste des Petits Ruminants |
| PPP | Public Private Partnership |
| RUWASA | Rural Water Supply and Sanitation Agency |
| RVF | Rift Valley Fever |
| SACCOS | Savings and Credit Co-operative Societies |
| SZK | Sekta Za Kilimo |
| TAA | Tanzania Airport Authority |
| TAFIRI | Tanzania Fisheries Institute |
| TANESCO | Tanzania Electricity Supply Company |
| TANROADS | Tanzania National Roads Agency |
| TARI | Tanzania Agricultural Research Institute |
| TALIRI | Tanzania Livestock Research Institute |
| TARURA | Tanzania Rural and Urban Roads Agency |
| TAZARA | Tanzania Zambia Railway Authority |
| TBS | Tanzania Bureau of Standards |
| TFRA | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority |
| TIC | Tanzania Investment Center |
| TLMP | Tanzania Livestock Master Plan |
| TMDA | Tanzania Medicines and Medical Devices Authority |
| TPA | Tanzania Ports Authority |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |


## KAULI YA MHESHIMIWA MKUU WA MKOA



Ni furaha yangu kuwasilisha kwenu Wadau wa maendeleo Mpango Mkakati wa Mkoa wa Kuendeleza Sekta za Kilimo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (2020-2025). Mpango Mkakati huu ni matokeo ya ushirikishwaji wa wadau mbalimbali kwa ajili ya kuchochea ustawi wa Mkoa wetu kwa kuhakikisha usalama wa chakula na kuongeza kipato.

Mpango mkakati huu, unaonesha Dira na Adhma yetu ya kufanya mapinduzi makubwa katika sekta za kilimo kwa kuweka mazingira salama na tulivu kwa wadau wote kushiriki ipasavyo. Mazingira makuu ya uandaaji na utekelezaji wa mpango mkakati huu yamejengwa kwa kuzingatia vipaumbele vya wadau wote katika ngazi ya Mkulima, Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa na Taifa kwa ujumla. Ni jukumu letu sasa sisi Viongozi kuanzia ngazi ya chini hadi Taifa kushirikiana na Wadau wote wa maendeleo kuanzisha safari hii ya mapinduzi ya sekta ya kilimo kwa kuweka mipango kazi na rasilimali zitazowezesha utekelezaji wa mpango mkakati huu.

Mwisho, nipende kuwahakikisha Wadau wote wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi kuwa Uongozi wa Mkoa na Wilaya zake utaweka mazingira salama na rafiki ya kuhakikisha kuwa sekta za kilimo (kilimo, mifugo, uvuvi na ushirika) zinakua na kuchangia ipasavyo katika usalama wa chakula pato la Mkoa na Taifa kwa ujumla. Niwatakie utekelezaji mwema wa Mpango Mkakati wa Kuendeleza Sekta za Kilimo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo 2020-2025.



**Albert Chalamila**
**Mkuu wa Mkoa**
**MBEYA**

## SHUKRANI



Mpango Mkakati wa Kuendeleza Sekta za Kilimo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (**2020-2025**) ni matokeo ya ushirikishwaji wa wadau katika kupanga na kutekeleza mapinduzi chanya ya sekta hizi. Maandalizi ya mpango mkakati huu umezingatia Mpango Mkakati wa Mkoa (**2018/2019-2022/2023**), na Mipango ya Taifa ikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano **(2016-2021),** Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili II **(2018-2023),** Mpango Kabambe wa Mifugo – TLMP (**2018-2022**), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi **(2020-2025),** Dira ya Maendeleo ya Taifa **2025**, Sera ya Kilimo ya Mwaka **2013**, Sera ya Mifugo ya Mwaka **2006**, Sera ya Uvuvi ya Mwaka **2015,** Sera ya Ushirika ya Mwaka 2002 na Miongozo mbalimbali kwa ajili ya kutoa Dira ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa kipindi cha Miaka mitano ijayo **(2020-2025)**.

Mpango Mkakati huu umezingatia vipaumbele vya Mkoa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita **(2015-2020)** na matarajio ya kuviboresha kwa kipindi cha miaka mitano ijayo **(2020-2025)**. Mazao yaliyolengwa ni Mpunga, Mahindi, Ndizi, Viazi Mviringo, Maharage, Mboga/Matunda, Mazao ya Mbegu za Mafuta (Alizeti, na Michikichi), Kahawa, Korosho, Chai, Tumbaku, Kakao, Pareto, na kwa Mifugo na Uvuvi ni Maziwa, Nyama (ng'ombe), Mbuzi na Kondoo, Kuku, Ngozi na Samaki. Aidha, uchaguzi wa vipaumbele katika mpango mkakati umeangalia pamoja na mambo mengine mchango wa zao husika katika usalama wa chakula, malighafi kwa viwanda, mchango katika ajira, upatikanaji wa soko na upatikanaji wa teknolojia inayoweza kuchangia ongezeko la uzalishaji na tija. Pamoja na mazingatio haya mpango mkakati umezingatia maelekezo ya Viongozi katika ngazi zote na kanda za uzalishaji zinazopatikana kwenye mkoa wetu.

Mwisho, niwashukuru sana Wadau wote walioshiriki kwa hali na mali kuwezesha uandaaji wa mpango mkakati huu. Kipekee niwashukuru Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mheshimiwa Albert Chalamila kwa kuridhia mchakato huu, Kaimu Katibu Tawala Msaidizi anayesimamia Uchumi na Uzalishaji Ndg. Said J. Maditto, Maafisa Kilimo Ndg. Wilfred C. Kayombo, Ndg. Thadey Ngambila, Ndg. Marianus Ngui, Daktari wa

Mifugo Ndg. Samora Mshang'a, Afisa Uvuvi Ndg. Adam Mhagama, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa Bi. Anjela Maganga, Maafisa Ushirika, Ndg. Biezery Malila na Bi. Irene Luoga na Ofisi za Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine wa sekta za kilimo kwa ushiriki wenu katika kukamilisha maandalizi ya mpango mkakati huu. Ahsanteni Sana!

Nawatakia utekelezaji mwema.

……………………………

**M. A. Mtunguja**
**Katibu Tawala Mkoa**
**MBEYA**

## DIBAJI

Kwa mujibu wa Sheria Na. 19 ya 1997 (Tawala za Mikoa) na Miongozo mbalimbali, Sekretarieti ya Mkoa ina majukumu ya kiutawala na ya kimaendeleo. Sekretarieti ya Mkoa inategemewa kuongoza na kuwa kiungo kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa “(OR-TAMISEMI) pamoja na Wizara za Kisekta ngazi ya Taifa.

Katika kusimamia maendeleo Sekretarieti ya Mkoa imeandaa Mpango Mkakati kwa Wadau wa maendeleo ambao utoa majukumu kwa kila mdau katika kuendeleza sekta za kilimo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (2020-2025). Mgawanyo wa majukumu kwa kila mdau yamezingatia wajibu wa kisheria wa Sekretarieti ya Mkoa wa kusimamia majukumu ya kiutawala na maendeleo ya wananchi ndani ya mkoa.

Hivyo, uandaaji wa Mpango Mkakati umezingatia ushiriki wa wadau wa sekta za kilimo wa ndani na nje ya Mkoa. Jambo hili limefanyika kwa kuangalia mazingira ya ndani na nje ya taasisi yetu, uimara na udhaifu tulionao ndani ya Mkoa katika kusimamia majukumu ya msingi kisheria, fursa na changamoto zinazoweza ama kuwa mtaji au vikwazo vya ufanisi wa lengo kuu tarajiwa.

Ushiriki wa wadau wote katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa kuendeleza Sekta Za Kilimo utachangia kufikia Dira na Dhima ya Mkoa wetu kupitia malengo, shabaha, shughuli zitakazotekelezwa kupitia rasilimali zitakazotengwa na Wadau ndani ya miaka mitano ijayo. ***Kilimo Biashara kwa Maendeleo*** (***Agribusiness for Development***) ndio itakuwa tamko letu katika utekelezaji wa mpango mkakati huu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo 2020-2025.

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Mahali ulipo Mkoa

Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa inayopatikana Nyanza za Juu Kusini kwenye Latitude 7ºna 9º31' kusini mwa Ikweta na kati ya Longitudi 32º na 35º Mashariki mwa Greenwich. Mkoa unapakana na Jamhuri ya Malawi na Songwe kwa upande wa Kusini na Magharibi, Tabora na Singida kwa upande wa Kaskazini na Mikoa ya Iringa na Njombe kwa upande wa Mashariki. Kwa sasa mpaka wa Kasumulu ndio lango la kuingia na kuelekekea Jamhuri ya Malawi.

### 1.2 Eneo, Idadi ya Watu

Mkoa wa Mbeya una eneo la kilometa za mraba 35,960 zilizogawanyika katika Wilaya 5 na Halmashauri 7. Wilaya zimegawanyika katika Tarafa 15, Kata 179, Vijiji 533 na Mitaa 181. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 Mkoa wa Mbeya ulikuwa na watu 1,708,548 na kati yao wanawake ni 889,690 na wanaume ni 818,858. Maoteo ya idadi ya watu katika mwaka 2020 ni 2,136,614 ambapo wanawake ni 1,102,171 na wanaume 1,034,443. Wastani wa ongezeko la idadi ya watu ni 2.4% kwa mwaka.

### 1.3 Pato la Mkoa

Uchumi wa Mkoa unategemea kilimo, ufugaji, uchimbaji madini, uvunaji mazao ya maliasili, biashara, uzalishaji viwandani na ajira katika Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi. Aidha, pato la Mkoa limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka ambapo mwaka 2015 lilikuwa Shilingi trilioni 5.3037, mwaka 2016 Shilingi trilioni 6.0914, mwaka 2017 Shilingi trilioni 6.6632, mwaka 2018 Shilingi trilioni 7.2962 na mwaka 2019 pato la mkoa limefikia Shilingi trilioni 7.8499.

Aidha, wastani wa pato la mtu limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka ambapo mwaka 2015 lilikuwa Shilingi 2,882,915, mwaka 2016 Shilingi 3,233,353, mwaka 2017 Shilingi 3,322,819, mwaka 2018 Shilingi 3,524,025 na mwaka 2019 pato la mtu limeongezeka hadi kufikia Shilingi 3,673,999. Mkoa kwa mwaka 2019 ulichangia asilimia 5.61 ya Pato la Taifa ukishika nafasi ya nne.

### 1.4 Hali ya Ulinzi na Usalama

Hali ya Ulinzi na Usalama katika Mkoa wa Mbeya kwa ujumla ni shwari. Matukio machache ya uvunjifu wa amani yanadhibitiwa na kushughulikiwa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama kwa mujibu wa Sheria za Nchi. Aidha, hali ya kisiasa katika Mkoa ni tulivu na wananchi wanaendelea kufanya shughuli zao za maendeleo kwa amani na utulivu.

## 1.5 Kanda za Uzalishaji

Mkoa kwa ujumla umegawanyika katika kanda kuu tatu kulingana na aina ya udongo, uoto wa asili, mwinuko kutoka usawa wa bahari huku sehemu kubwa ya Mkoa ikiwa imetawaliwa na uwepo wa udongo uliotokana na milipuko ya volcano na uwepo wa Bonde la Ufa. Kanda hizi ndizo zinazotambulisha aina ya shughuli ya kiuchumi hususani kilimo inayoweza kufanyika kama inavyofafanuliwa hapa chini: -

### 1.5.1 Ukanda wa Juu

Ukanda huu unasifika kwa kuwa na mvua za kutosha, udongo wenye rutuba na ni maarufu kwa shughuli za kilimo hivyo kuwa na wakazi wengi kuliko kanda zingine. Ukanda huu unapatikana maendeo ya Bonde la Usangu, Uwanda wa Kati wa Mbeya, Safu za Milima ya Mporoto na Ilembo na maeneo ya Kusini mwa Rungwe, Kusini na Kaskazini mwa Kyela. Ukanda huu uko kati ya mwinuko wa kati ya Mita **1,500** na **2,400** juu ya usawa wa bahari. Maeneo haya hupata mvua kwa mwaka wastani wa zaidi ya Milimita **2,500**. Maeneo haya ni maarufu kwa kilimo cha Mahindi, Mpunga, Maharage, Karanga, Ngano, Viazi, Kahawa, Ndizi, Chai na Kakao. Maeneo haya pia ni maarufu kwa ufugaji wa mifugo.

### 1.5.2 Ukanda wa Kati

Ukanda wa Kati hupatikana kwenye mwinuko wa kati ya mita **800** hadi **1,500** juu ya usawa wa bahari. Ukanda huu hupata mvua za wastani wa milimita **700** na unajumuisha maeneo ya uwanda wa Usangu Kaskani na maeneo ya Isangati/Hezya iliyopo Mbeya. Kanda hii ni hustawisha Mahindi, Mtama, Ulezi, Pamba, Choroko, Karanga, Mihogo, Maharage na Mpunga pamoja na shughuli za ufugaji wa ng’ombe, mbuzi na kondoo.

### 1.5.3 Ukanda wa Chini

Ukanda wa chini hupatikana kwenye mwinuko wa Mita **500** hadi **1,000** juu ya usawa wa bahari. Ukanda huu hujumuisha maeneo ya Kaskazini na Kati mwa Wilaya ya Chunya, Safu za Msangaji na ukanda wa chini wa Kyela kuelekea Ziwa Nyasa. Maeneo yaliyopo kwenye ukanda huu hupata mvua chini ya wastani wa Milimita **1,000** kwa mwaka na ardhi yake haina rutuba ya kutosha. Hata hivyo baadhi ya maeneo katika Wilaya ya Kyela huweza kupata mvua zaidi ya milimita **2,500** kwa mwaka. Shughuli za kiuchumi katika maeneo hay ani pamoja na kilimo cha Mahindi, Tumbaku, Mtama, Ulezi, Mihogo, Karanga, Kakao, Korosho, Michikichi, Mpunga na Ndizi. Pia, Wakazi wa maeneo haya hufuga ng’ombe, mbuzi na kondoo.

## SURA YA PILI

## UCHAMBUZI WA HALI HALISI NA WADAU

### 2.0 Utangulizi

Uchambuzi wa Wadau wa Maendeleo na Taasisi umefanyika ili kuona hali halisi ya mazingira ya ndani na nje ya taasisi yetu, aina ya wateja, aina ya huduma na uwezo wa wadau/taasisi katika kusimamia mapinduzi ya sekta za kilimo ifikapo 2025. Uchambuzi umefanyika katika hatua kuu mbili ambazo ni muhimu sana ili kuona ni mambo yapi na njia zipi zitumike katika utekelezaji wa mpango mkakati. Uchambuzi wa kwanza umeangalia mambo muhimu ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kisheria na teknolojia na hatua ya pili ilikuwa kuangalia mazingira ya ndani ya taasisi (uimara na udhaifu) na ya nje (fursa na vikwazo) ya mkoa wetu.

### 2.1. Uchambuzi wa Wadau

Uchambuzi wa wadau umefanyika ili kujibu maswali kadhaa yakiwemo: Wadau wetu ni kinani? Je, huduma zipi wanatoa? Nini matarajio kutoka kwenye mpango? Katika uchambuzi huo mpango mkakati umebainisha wadau watakaohusika katika utekelezaji wake kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1:** Uchambuzi wa Wadau wa Sekta za Kilimo

| MDAU | HUDUMA ANAZOTOA | MATARAJIO KUTOKA KWENYE MPANGO | KIPIMO CHA MATARAJIO |
|---|---|---|---|
| Wakulima/Wafugaji/Wavuvi | 1. Kulima, kufuga na Uvuvi<br>2. Nguvu kazi<br>3. Usindikaji<br>4. Kujiunga kwenye ushirika | 1. Upatikanaji wa pembejeo bora kwa wakati<br>2. Utawala bora kwenye vyama vya ushirika<br>3. Huduma bora za ugani Upatikanaji wa masoko ya uhakika na shindani<br>4. Upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu | Juu |
| Halmashauri | 1. Kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza sekta za kilimo<br>2. Utawala bora<br>3. Huduma za Ugani<br>4. Ufuatiliaji na tathmini<br>5. Utekelezaji wa Sera, Sheria, Miongozo na program za kitaifa<br>6. Ulinzi na Usalama | 1. Mazingira bora na rafiki ya uwekezaji<br>2. Sheria ndogo zilizoboreshwa<br>3. Upatikanaji wa taarifa kwa ubora na wakati sahihi<br>4. Ushirikishwaji wa wadau katika vikao<br>5. Kuwaunganisha wakulima na wadau wengine<br>6. Uzingatiaji wa utawala bora | Juu |

| MDAU | HUDUMA ANAZOTOA | MATARAJIO KUTOKA KWENYE MPANGO | KIPIMO CHA MATARAJIO |
|---|---|---|---|
| Maafisa Ugani | 1. Kuwa kiungo kati ya wakulima, watafiti na wadau<br>2. Kutafiti masoko ya mazao<br>3. Kushiriki tafiti za maendeleo ya sekta za kilimo | 1. Mazingira bora ya utoaji huduma za ugani.<br>2. Elimu rejea za ugani.<br>3. Motisha kwa wataalam wa ugani<br>4. Ushirikishwaji katika vikao vya wadau wa Sekta za Kilimo<br>5. Kupatiwa yatokanayo/majibu ya Tafiti zinazofanywa | Juu |
| Wauzaji/Wasambazaji Pembejeo za Kilimo | 1. Upatikanaji wa pembejeo bora<br>2. Kushiriki kutoa huduma za ugani | 1. Mazingira bora na rafiki ya upatikanaji wa pembejeo<br>2. Ushiriki kamilifu katika tafiti za kilimo<br>3. Bei rafiki ya pembejeo<br>4. Uzingatiaji wa ubora na upatikanaji wa pembejeo | Juu |
| Taasisi za Fedha/ Benki | 1. Mikopo ya masharti nafuu<br>2. Kushiriki kutoa huduma za ugani | 1. Ushiriki katika vikao vya wadau<br>2. Uzingatiaji wa utawala bora<br>3. Mazingira bora ya uwekezaji | Wastani |
| Vyuo vya utafiti na mafunzo (TARI, TAFIRI, TARILI, MATI, Vyuo Vikuu n.k) | 1. Kufanya tafiti zenye tija<br>2. Kushiriki kutoa huduma za Ugani<br>3. Ushiriki katika uibuaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo<br>4. Kuzalisha wataalam na wagani katika sekta za kilimo<br>5. Uingizaji wa Teknolojia rahisi katika Uzalishaji | 1. Mazingira bora ya utendaji kazi<br>2. Utoaji wa taarifa za tafiti kwa muda na kwa njia rafiki kwa wakulima/wafugaji na wadau wengine<br>3. Kushiriki katika vikao vya ushauri na maamuzi juu ya sekta za kilimo<br>4. Kushiriki katika kutoa tafiti na bunifu za uongezaji thamani za mazao | Wastani |

| MDAU | HUDUMA ANAZOTOA | MATARAJIO KUTOKA KWENYE MPANGO | KIPIMO CHA MATARAJIO |
|---|---|---|---|
| Taasisi za udhibiti ubora (TBS, TFRA, TMDA, n.k) | 1. Usimamiaji wa Sheria na Miongozo ya ubora wa bidhaa<br>2. Usajili na utambuzi wa Wadau | 1. Mazingira bora na udhibiti ubora<br>2. Uzingatiaji wa sheria husika kwa wadau<br>3. Ushirikishwaji katika vikao | Wastani |
| Mamlaka ya Hali ya Hewa | 1. Kutoa taarifa za hali ya hewa kwa wadau kwa wakati<br>2. Kushiriki kutoa huduma za ugani | 1. Utoaji wa taarifa za hali ya hewa kwa muda na kwa njia rafiki kwa wakulima/wafugaji na wadau wengine<br>2. Ushirikishwaji katika vikao<br>3. Mazingira bora ya kazi | Juu |
| AZAKI na Vyama vya Ushirika | 1. Uandaji wa maandiko miradi<br>2. Kushiriki kutoa huduma za Ugani<br>3. Kushauri masuala ya kisera<br>4. Mikopo kwa wanachama | 1. Mazingira bora ya kazi<br>2. Ushirikishwaji katika vikao vya Wadau<br>3. Ushirikishwaji katika upangaji na utekelezaji wa miradi<br>4. Utawala bora katika Vyama vya Ushirika<br>5. Uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi | Wastani |
| Vyombo vya Habari | 1. Uhabarishaji wa Umma<br>2. Uibuaji wa miradi na mahitaji ya jamii<br>3. Uhamasishaji amani na utulivu katika jamii | 1. Utoaji wa taarifa sahihi na kwa muda<br>2. Ushirikishwaji katika shughuli za maendeleo<br>3. Mazingira bora ya kazi<br>4. Uwazi na uwajibikaji katika kuwahabarisha wadau<br>5. Ushirikishwaji katika vikao vya wadau | Wastani |
| Viongozi wa Kisiasa na Dini | 1. Utekelezaji wa Ilani<br>2. Uhamasishaji wa shughuli za maendeleo<br>3. Uhamasishaji amani na utulivu<br>4. Ushauri kwa Serikali<br>5. Kuchangia shughuli za maendeleo | 1. Ushirikishwaji katika vikao vya maendeleo ndani ya Mkoa<br>2. Ulinzi na Usalama<br>3. Mazingira yenye haki na usawa kwa makundi yote<br>4. Ushirikishwaji katika matukio ya kisiasa, kidini na kijamii | Wastani |

| MDAU | HUDUMA ANAZOTOA | MATARAJIO KUTOKA KWENYE MPANGO | KIPIMO CHA MATARAJIO |
|---|---|---|---|
| Wizara za Kisekta | 1. Kutunga Sera, Sheria na Miongozo<br>2. Kusambaza Sera, Sheria na Miongozo<br>3. Kuunganisha Mikoa, Halmashauri na wadau<br>4. Kutoa Rasimali kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wadau<br>5. Kujenga uwezo kwa Mikoa na MSM | 1. Uwasilisha wa taarifa na maelekezo kwa wadau kwa muda<br>2. Ushiriki katika utekelezaji wa miradi<br>3. Ushirikiano chanya na wadau wa maendeleo | Wastani |
| Wahisani/Waweke zaji | 1. Uandaaji wa maandiko miradi<br>2. Kupendekeza maeneo ya mashirikiano<br>3. Uzingatiaji wa Sheria na Utawala bora | 1. Mazingira bora ya kazi<br>2. Utoaji wa taarifa sahihi kwa wadau na kwa muda muafaka<br>3. Utambuzi wa juhudi na kazi za wadau<br>4. Uzingatiaji wa utawala bora na sheria<br>5. Uwajibikaji na uwazi katika masuala ya fedha<br>6. Ushiriki katika vikao vya wadau | Juu |
| Taasisi Wezeshi (TRA, TANESCO, TARURA, TANROADS, RUWASA, TIC, OSHA, NEMC, LATRA, n.k | 1. Usajili na utambuzi wa Wadau | 1. Mazingira bora ya uwezeshaji shughuli za wadau<br>2. Uzingatiaji wa sheria husika kwa wadau<br>3. Ushirikishwaji katika vikao vya wadau | Wastani |
| Vyombo vya Ulinzi na Usalama | 1. Ulinzi na Usalama | 1. Mazingira bora ya kazi<br>2. Mazingira ya haki na usawa kwa makundi yote ya jamii | Juu |
| Vyombo vya usafiri na usafirishaji (TPA, TAA, TAZARA, n.k) | 1. Kusafirisha Pembejeo na Mazao ya sekta za kilimo<br>2. Kutunza ubora wa mazao | 1. Mazingira bora ya utendaji<br>2. Upatikanaji wa mizigo ya kutosha ya kusafirisha<br>3. Kushiriki vikao vya maendeleo ndani ya Mkoa | Wastani |

### 2.2. Uchambuzi wa Hali Halisi

Mpango Mkakati wa SZK umefanyika kwa kuangalia Uimara, udhaifu, fursa na changamoto zilizopo ndani na nje ya mazingira ya taasisi na mwisho kuwezesha uwekaji wa mikakati kwa kila eneo kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2:** Uchambuzi wa Hali Halisi Mkoa wa Mbeya

| | **UIMARA** | **UDHAIFU** |
|---|---|---|
| | 1. Uwepo wa nguvu kazi ya uzalishaji mazao.<br>2. Upatikanaji wa teknolojia za uongezaji thamani mazao.<br>3. Uwepo wa taasisi za elimu ya juu na utafiti.<br>4. Uwepo wa wataalam wa ugani katika sekta za kilimo.<br>5. Uwepo wa miundombinu bora ya usafiri na usafirishaji.<br>6. Uwepo wa Ziwa Nyasa na vyanzo vya maji vya uhakika kwa mwaka mzima.<br>7. Uwepo wa vyombo vya Habari vyenye kusikika mkoa mzima<br>8. Uwepo kwa utulivu na usalama kwa makundi yote ndani ya jamii. | 1. Kilimo cha mazoea.<br>2. Upotevu mkubwa wa mazao wakati na baada ya kuvuna.<br>3. Uwepo wa visumbufu na magonjwa ya mazao na mifugo<br>4. Uwepo wa migogoro / ubadhilifu kwenye baadhi ya vikundi/vyama vya ushirika.<br>5. Ubovu wa miundombinu kwenye skimu za umwagiliaji.<br>6. Kilimo kuwa tegemezi cha mvua kwa kiwango cha juu.<br>7. Masoko holela na yasiyoshindani kwa baadhi ya mazao ya kipaumbele. |
| **FURSA** | **MIKAKATI: UIMARA+FURSA** | **MIKAKATI: UDHAIFU+FURSA** |
| 1. Ardhi nzuri na yenye rutuba<br>2. Hali ya hewa nzuri inayostawisha mazao mbalimbali.<br>3. Uwepo wa masoko ya ndani na nje ya nchi.<br>4. Uwepo wa Sheria, Sera, Programu na Miongozo ya uendelezaji wa sekta za kilimo<br>5. Uwepo wa taasisi za elimu ya kati na juu zinazohudumia sekta za kilimo<br>6. Uwepo wa Ofisi za | 1. Kuimarisha matumizi sahihi ya pembejeo bora za kilimo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na tija<br>2. Kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogo vya usindikaji wa mazao<br>3. Kuhamasisha kilimo cha mboga na matunda kwa ajili ya soko la ndani na nje<br>4. Kuimarisha huduma za miundombinu ya vyumba baridi kwa ajili ya mazao ya bustani.<br>5. Kuhamsisha sekta binafsi kuwekeza kwenye kiwanda cha mbolea ndani ya mkoa<br>6. Kutoa elimu rejea kwa maafisa ugani kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na tija | 1. Kuhamasisha kilimo hifadhi na Rafiki wa mazingira.<br>2. Kupima afya ya udongo kwenye maeneo ya uzalishaji<br>3. Kutenga na kupima maeneo ya malisho<br>4. Kuhamasisha uhimilishaji wa mifugo ili kuboresha koosafu/mbari<br>5. Kutoa mafunzo kwa wataalam wa ugani na wakulima ili kuongeza uzalishaji na tija.<br>6. Kutunga/kuhuisha sheria ndogo za |

| | UIMARA | UDHAIFU |
|---|---|---|
| Taasisi wezeshi za Kanda ndani ya Mkoa<br>7. Uwepo wa ustahimilivu na utulivu wa kisiasa | 7. Kuajiri Maafisa Ugani kwenye maeneo ya kilimo<br>8. Uanzishwaji wa mifumo rafiki na shindani ya masoko kwa mazao ya kipaumbele.<br>9. Kuhamasisha uanzishaji wa vikundi/vyama vya ushirika.<br>10. Kuhamasisha ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba | kuendeleza sekta ya kilimo.<br>7. Ukusanyaji na matumizi yataarifa za hali ya hewa.<br>8. Kuandaa kalenda za mazao ya kimkakati.<br>9. Kuanzisha vituo maalum ya ukusanyaji/upimaji wa mazao ya kilimo. |
| **TISHIO** | **MIKAKATI: UIMARA+TISHIO** | **MIKAKATI: UDHAIFU+TISHIO** |
| 1. Mabadiliko ya tabia nchi<br>2. Mwingiliano wa Siasa katika utekelezaji wa shughuli za kilimo<br>3. Mabadiliko ya Sheria, Sera na Miongozo<br>4. Mlipuko wa magonjwa ya mazao na mifugo | 1. Kuhamasisha kilimo shadidi kwenye skimu za umwagiliaji ili kupunguza upotevu wa maji<br>2. Kuimarisha na kuboresha miundombinu kwenye skimu za umwagiliaji<br>3. Uimarishaji wa utawala bora na ushirikishwaji wa jamii katika miradi ya kilimo | 1. Kuhamasisha kilimo mseto na rafiki wa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi<br>2. Kuhamasisha na kuanzisha bima ya mazao<br>3. Utayari wa kudhibiti na kukabiliana na maafa/majanga |

## SURA YA TATU

## DIRA, DHIMA, MISINGI YA TAASISI NA MALENGO

### 3.0 Utangulizi

Mpango Mkakati wa Kuendeleza Sekta Za Kilimo umeandaliwa kwa kuzingatia Dira, Dhima na Misingi ya Taasisi yaliyowekwa na Mkoa kwenye Mpango Mkakati wa Mkoa wa mwaka 2018/2019 – 2021/2022.

### 3.1. Dira

"Kuwa Taasisi mahiri na inayozingatia Utawala bora katika kusimamia maendeleo"

### 3.2. Dhima

"Kuwezesha na kujenga uwezo wa Halmashauri kusimamia maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi kwa kutumia rasilimali zilizopo na za Wadau kwa ajili ya kupunguza umasikini na kuongeza ukuaji na ustawi wa maendeleo ya wananchi"

### 3.3. Misingi ya Taasisi

Katika kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kuendeleza Sekta za Kilimo kwenye Mkoa, Sekretarieti itazingatia vitu vifuatavyo: -

i. Usawa na haki
ii. Heshima na Utu
iii. Uwazi na uwajibikaji
iv. Ufanisi na Weledi
v. Utawala Bora
vi. Ubunifu
vii. Ufanyaji kazi kitimu
viii. Kujali wateja
ix. Hamasa ya Wateja na Watumishi

### 3.4. Malengo ya Mpango Mkakati

#### 3.4.1. Lengo Kuu

Kufanya mapinduzi katika Sekta Za Kilimo (Mazao, Mifugo, Uvuvi na Ushirika) kwa kuongeza uzalishaji na tija, kufanya kilimo shindani na cha kibiashara ili kuhakikisha usalama wa chakula, kipato na lishe bora kwa wananchi.

#### 3.4.2. Malengo Mahususi

i. Kusimamia mapinduzi ya kilimo ili kuhakikisha kinakuwa chenye tija na kinachotumia teknolojia za kisasa.
ii. Kuleta mabadiliko makubwa katika ufugaji wa kisasa wenye kuzingatia kinga, tiba na utafiti ili kuongeza uzalishaji na tija kwa ajili ya ustawi wa wananchi.
iii. Kuhakikisha sekta ya uvuvi inaimarika kwa kuongeza matumizi ya sayansi na teknolojia ya uvuvi endelevu ili kuwa shindani na yenye kuchangia kwa kiasi kikubwa usalama wa chakula na kipato.
iv. Kuimarisha huduma za ushirika wa kisasa na unaowajibika kwa wadau kwenye makundi ya uzalishaji mali na uongezaji thamani za mazao na huduma za kilimo

## SURA YA NNE

## MPANGO MKAKATI WA MKOA WA KUENDELEZA SZK MWAKA 2020 – 2025

### 4.0 Utangulizi

Mkakati wa Mkoa katika kuendeleza SZK umeandaliwa kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Mkoa 2018/2019 – 2021/2022, na Mipango ya Taifa ikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano **(2016-2021),** Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili II **(2018-2023),** Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi **(2020-2025),** Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Sera ya Kilimo ya Mwaka 2013, Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006, Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015, Sera ya Ushirika ya Mwaka 2002 na miongozo mbalimbali kwa ajili ya kutoa Dira ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa kipindi cha Miaka mitano ijayo **(2020-2025)**.

Kufuatia utafiti uliofanywa na *NBS* 2015, SZK zinachangia asilimia **74.7** ya Pato la Mkoa na kuajiri zaidi ya asilimia **80** ya Wakazi katika Minyororo ya Thamani ya Bidhaa na Huduma za SZK. Kwa hiyo, Mkakati wa Mkoa wa Kuendeleza SZK kwa Kipindi cha Mwaka 2020 – 2025 utasaidia kuleta mapinduzi ya kilimo. Hii ni pamoja na kuongeza tija na kipato kwa Wadau waliopo katika ngazi mbalimbali za minyororo ya thamani ya SZK, kuboresha maisha yao, kuwezesha usalama wa chakula na lishe, pia kuchangia pato la Mkoa na Taifa.

Kwa miongo kadhaa juhudi kubwa iliwekwa katika kuongeza matumizi ya sayansi na teknolojia katika mazao ya kipaumbele ya kilimo, mifugo na uvuvi ambayo yaliainishwa kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

i. Mchango katika usalama wa chakula;
ii. Zao linalolimwa na wakulima/wafugaji wadogo walio wengi;
iii. Umuhimu katika soko la ndani na nje ya nchi;
iv. Mchango katika kuchangia malighafi na ajira katika viwanda;
v. Mchango katika ajenda ya maendeleo ya Taifa ya viwanda na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano;
vi. Upatikanaji wa teknolojia za kuongeza tija na faida; na
vii. Miradi inayoendelea kukamilishwa.

Juhudi hizi zimewezesha ongezeko la uzalishaji wa mazao na kutoa mchango mkubwa katika kapu la chakula, ajira na kuongeza malighafi za viwanda lakini tija ya uzalishaji kwa eneo/mnyama bado ni ndogo. Kwa madhumuni haya Mkoa unaamini kuwa zipo changamoto nyingi zinazowakabili Watendaji (*Actors*) mbalimbali katika minyororo ya SZK kiasi cha kufanya uzalishaji wa mazao kutofikia tija inayotakiwa. Kwa kuzingatia hali hii Mkakati huu utawezesha wazalishaji na wasindikaji kuwa na dira ya kutekeleza Kilimo Biashara kwa Maendeleo (*Agribusiness for Development).*

Kwa muktadha huu uandaaji wa Mkakati huu umezingatia vipaumbele vya Mkoa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita **(2015-2020)** na matarajio ya kuviboresha/kuongeza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo **(2020-2025)**. Mazao yaliyolengwa ni Mpunga, Mahindi, Ndizi, Viazi Mviringo, Maharage, Mboga/Matunda, Mazao ya Mbegu za Mafuta (Alizeti, na Michikichi), Kahawa, Korosho, Chai,

Tumbaku, Kakao, Pareto, na kwa Mifugo na Uvuvi ni Maziwa, Nyama (ng'ombe), Mbuzi na Kondoo, Kuku, Ngozi na Samaki.

Msingi wa ufanisi wa utekelezaji wa mkakati huu utategemea vigezo vifuatavyo:-

i. Uwajibikaji wa viongozi katika kubadili mtazamo mpana wa SZK;
ii. Uratibu mpana wa SZK kwa wadau wote (kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini kwa mtazamo mpana) katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Tarafa, Kata na Vijiji katika ushirikishwaji wa wadau katika kupanga na kutekeleza, kujenga uwezo na uwekezaji;
iii. Uwekezaji katika ngazi ya Wilaya kwa kuzingatia vipaumbele katika mnyororo wa thamani wa zao husika;
iv. Kutumia teknolojia za kisasa za habari na mawasiliano kwa ufanisi wa uratibu na ukusanyaji takwimu kwa ajili ya matumizi ya wadau;
v. Kujenga uwezo wa Wakulima,Wafugaji na Wavuvi pia kuimarisha vikundi/vyama vya ushirika ili waweze kushiriki kikamilifu katika kujiletea maendeleo.
vi. Kuendeleza mfumo endelevu wa uzalishaji na matumizi ya maliasili kwa kuhamasisha kilimo hifadhi na rafiki wa mazingira, urutubishaji wa ardhi, ufugaji wa mifugo inayoendana na maeneo ya malisho, ufugaji wa samaki na uvuvi endelevu wenye tija; na
vii. Uimarishaji wa Utawala bora na uwajibikaji katika usimamizi wa SZK katika ngazi zote.

## 4.1 Sekta ya Kilimo 2015-2020 na Mpango Mkakati wa 2020-2025

### 4.1.1 Eneo la Kilimo

Mkoa una jumla ya hekta **3,519,698.70** ambapo eneo linalofaa kwa ajili ya kilimo ni hekta **1,749,821.20** sawa na asilimia **49.72.** Kwa sasa wakulima wanalima wastani wa hekta **577,054** sawa na asilimia **33 (Jedwali Na. 3)**

**Jedwali Na. 3:** Eneo la Kilimo

| Halmashauri | Eneo (Ha) | Eneo kwa Hekta | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Linalofaa | Linalolimwa | Linalolimwa (%) |
| Busokelo | 84,712.7 | 46,824.2 | 45,521 | 97 |
| Chunya | 1,315,000 | 1,035,400 | 93,249 | 9 |
| Kyela | 132,200 | 55,000 | 52,000 | 94 |
| Mbarali | 1,600,000 | 321,500 | 165,230 | 51 |
| Mbeya (W) | 243,200 | 189,818 | 119,778 | 63 |
| Mbeya Jiji | 21,400 | 8,890 | 8,887 | 100 |
| Rungwe | 123,186 | 92,389 | 92,389 | 100 |
| **Jumla kuu** | **3,519,698.70** | **1,749,821.20** | **577,054** | **33** |

**Chanzo:** Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mbeya, 2020

### 4.1.2 Uzalishaji wa Mazao (2015-2020)

Hali ya uzalishaji wa mazao imeendelea kuwa ya kuridhisha kiasi cha kuufanya Mkoa kutoa mchango mkubwa katika usalama wa chakula na kuongeza kipato kutokana na

kuuza mazao ndani na nje ya nchi. Kufanikiwa kwa Mkoa kumetokana na kuwepo kwa mazingira mazuri ya kilimo ikiwemo hali ya hewa na udongo wenye rutuba. Aidha, wakulima katika Mkoa wamehamasika katika shughuli za kilimo na wanayo nafasi kubwa ya chaguzi ya aina ya mazao wanayotaka kulima. Hii ni kutokana na kuwepo Kanda kuu tatu za kilimo (Kanda ya Juu, Kanda ya Kati na Kanda ya Chini) na kuwepo kwa miundombinu ya umwagiliaji ambayo inawawezesha kuzalisha kwa wingi mazao aina mbalimbali.

### 4.1.3 Umwagiliaji

Mkoa unatekeleza kilimo cha umwagiliaji ambacho kinatoa mchango mkubwa katika kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao ya chakula yakiwemo mpunga, mahindi, maharage na Mboga kwa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi pia kuwezesha kilimo kufanyika wakati wa kiangazi, katika baadhi ya maeneo.

Eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni jumla ya hekta 1**08,332** ambapo kati ya hizo eneo lililoboreshwa ni hekta **41.38.** Eneo linalomwagiliwa ni jumla ya hekta **54,606** ambapo kati ya hizo hekta **45,301** zinamwagiliwa wakati wa masika na hekta **9,305** wakati wa kiangazi. Mchanganuo wa maeneo hayo kiwilaya umeoneshwa katika Jedwali Na. 4

**Jedwali Na. 4:** Eneo (Ha) la Umwagiliaji

| Halmashauri | Linalofaa | Boreshwa | Mwagiliwa Masika | Mwagiliwa Kiangazi | Wanufaika wenye mashamba |
|---|---|---|---|---|---|
| Busokelo | 2,940 | 980 | 1,050 | 720 | 4,006 |
| Chunya | 1,154 | 151 | 647 | 276 | 441 |
| Kyela | 6,250 | 1,274 | 1,630 | 625 | 2,814 |
| Mbarali | 93,166 | 36,668 | 39,654 | 5,718 | 35,581 |
| Mbeya | 3,358 | 1,641 | 1,611 | 1,372 | 7,391 |
| MbeyaJiji | 964 | 667 | 559 | 594 | 1,968 |
| Rungwe | 500 | 0 | 150 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **108,332** | **41,381** | **45,301** | **9,305** | **52,201** |

**Chanzo:** Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mbeya,2020

Kilimo cha umwagiliaji kimewezesha kuongezea tija ya uzalishaji, kwa mfano kwa zao la mpunga ambalo ndilo zao kuu katika umwagiliaji, tija imeongezeka kutoka tani 3.5 – 8 kwa hekta kwa mkulima mmoja mmoja; wastani wa tani 5.75/ha.

### 4.1.4 Mazao ya Chakula ya Kipaumbele

Mazao ya kipaumbele ya chakula ni mahindi, mpunga, maharage, viazi mviringo na ndizi. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015-2020) uzalishaji wa mazao ya kipaumbele kwa ajili ya chakula umekuwa ni wa kuridhisha. Mkoa umezalisha wastani wa tani **641,386** za Mahindi, tani **354,439** za Mpunga, tani **81,087** za Maharage, tani **886,164** za Viazi Mviringo na tani **605,087** za ndizi (Jedwali Na. 5).

**Jedwali Na. 5:** Uzalishaji wa Mazao ya Kipaumbele (2015 -2020)

| MSIMU | Mazao ya Kipaumbele (Tani) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Mahindi | Mpunga | Maharage | Viazi (Mv) | Ndizi |
| 2015/2016 | 599,410 | 327,578 | 79,563 | 837,116 | 610,106 |
| 2016/2017 | 681,046 | 296,162 | 83,525 | 939,106 | 607,127 |
| 2017/2018 | 573,085 | 368,264 | 53,403 | 883,000 | 552,782 |
| 2018/2019 | 701,078 | 405,305 | 112,273 | 939,356 | 537,730 |
| 2019/2020 | 652,313 | 374,886 | 76,671 | 832,240 | 720,091 |
| **WASTANI** | **641,386** | **354,439** | **81,087** | **886,164** | **605,567** |

**Chanzo:** Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mbeya, 2020

### 4.1.5 Mahitaji na Usalama wa Chakula

Kwa kuzingatia hali ya uzalishaji wa mazao na vigezo vinavyotumika kupima hali ya usalama wa chakula ambavyo ni **Upatikanaji** (*Availability*), **Ufikikaji** (*Accessibility*), **Utumiaji** (*Utilization/Consumption*) na **Utengefu** (*Stability*), kuna utoshelevu wa chakula.

Aidha, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita hali ya usalama wa chakula kwa vigezo vyote ilikuwa ya kujitosheleza kiasi cha kwamba Mkoa umeweza kutumia wastani wa asilimia **16** ya kiasi cha chakula kilichokuwa kimezalishwa. Jedwali Na. 6 linaonesha wastani wa mahitaji ya chakula kwa mwaka kwa kipindi cha miaka mitano.

**Jedwali Na. 6:** Wastani wa Mahitaji ya Chakula/Mwaka/Tani (2015-2020)

| Msimu | Eneo-Limwa (Ha) | Uzalishaji | Watu (Idadi) | Mahitaji | Ziada | Mahitaji (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2015/2016 | 549,801 | 3,627,191 | 1,881,098 | 514,951 | 3,112,240 | 14 |
| 2016/2017 | 527,553 | 3,615,782 | 1,942,898 | 531,868 | 3,083,914 | 15 |
| 2017/2018 | 478,741 | 3,352,623 | 2,006,072 | 549,162 | 2,803,461 | 16 |
| 2018/2019 | 478,600 | 3,351,798 | 2,070,412 | 566,775 | 2,785,023 | 17 |
| 2019/2020 | 554,994 | 3,665,699 | 2,136,614 | 584,898 | 3,080,801 | 16 |
| **WASTANI** | **517,938** | **3,189,508** | **2,007,419** | **549,531** | **2,639,977** | **16** |

**Chanzo:** Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, 2020

### 4.1.6 Mazao ya Kimkakati ya Biashara

Mkoa una kilimo cha mazao ya Kimkakati ya biashara manne ambayo ni **Kahawa, Chai, Tumbaku** na **Korosho** yanayostawi sehemu mbalimbali Mkoani. Pamoja na mazao haya Mkoa umeweka mkakati wa kuendeleza mazao ya **Parachichi, Kakao, Alizeti, Pareto** na **Michikichi**.Takwimu zinaonesha (Jedwali Na. 7) katika kipindi cha 2015-2020 hali ya uzalishaji wa mazao hayo imekuwa siyo ya kuridhisha ukifananisha na eneo la uzalishaji.

**Jedwali Na. 7:** Uzalishaji wa Mazao ya Kimkakati ya Kibiashara (2015 -2020)

| MSIMU | Mazao ya Biashara ya Kipaumbele (Tani) | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kahawa | Chai | Korosho | Tumbaku | Kakao | Pareto | Michikichi | Parachichi | Alizeti |
| 2015/2016 | 3,725 | 29,570 | 345 | 10,417 | 10,537 | 1,925 | 2,204 | 278,106 | 28,286 |
| 2016/2017 | 3,097 | 23,575 | 327 | 10,972 | 9,589 | 1,507 | 2,292 | 277,197 | 17,506 |
| 2017/2018 | 2,468 | 17,581 | 309 | 11,527 | 9,973 | 2,390 | 2,100 | 262,875 | 41,168 |
| 2018/2019 | 3,594 | 17,581 | 309 | 11,960 | 9,346 | 2,390 | 2,160 | 277,838 | 23,149 |
| 2019/2020 | 3,445 | 19,831 | 139 | 8,915 | 9,209 | 3,759 | 2,489 | 150,204 | 23,672 |
| **WASTANI** | **3,266** | **21,628** | **286** | **10,758** | **9,731** | **2,394** | **2,249** | **249,244** | **26,756** |

**Chanzo:** Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mbeya na Halmashauri, 2020

Licha ya mazao haya ya kimkakati ya kibiashara kupewa kipaumbele katika Mkoa, uzalishaji na usindikaji wake bado upo chini. Hii ni kutokana na kutozingatia Kilimo Biashara katika kupambana na changamoto mbalimbali ikiwemo uwepo wa visumbufu vya mazao, matumizi hafifu ya pembejeo, uzee wa miti, matumizi ya mbegu/miche ya kienyeji na matumizi ya mbinu duni za uandaaji na usindikaji wa mazao haya. Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali, kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wa maendeleo zikiwemo;

i. Kuwahamasisha wakulima kutumia pembejeo za kilimo (mbegu bora, mbolea na viuatilifu) pamoja na matumizi ya zana bora za kilimo. ili kuongeza uzalishaji, tija na kupunguza upotevu.
ii. Kusimamia uagizaji na usambazaji wa mbolea kwa kufuata mfumo wa ununuzi wa pamoja (Bulk Procurement System – BPS) chini ya Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania (TFRA).

### 4.1.7 Mkakati wa Mkoa katika kuongeza uzalishaji na tija (2020-2025)

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri kuendelea kusimamia mapinduzi ya kilimo ili kuhakikisha kinakuwa chenye tija na kinachotumia teknolojia za kisasa kwa kufanya yafuatayo:-

***A. Kusimamia kikamilifu hifadhi na matumizi endelevu ya maji, ardhi ya kilimo na mazingira sambamba na kuongeza maeneo ya umwagiliaji kwa kufanya yafuatayo;***

i. Kuhamasisha kilimo hifadhi kwa wakulima 1,200,000.
ii. Kupanda miti 2,500,000 (Rafiki na Mazingira) kwenye vyanzo vya maji.
iii. Kuhamasisha wakulima katika skimu 160 za umwagiliaji kuchangia 5% ya wastani wa mavuno kwa ajili ya kuendeleza umwagiliaji
iv. Kuhamasisha kilimo shadidi kwenye skimu za umwagiliaji 70.
v. Kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 54,606 hadi hekta 75,000.
vi. Kupima afya ya udongo kwenye skimu za umwagiliaji 50.

***B. Kuongeza uzalishaji, tija na faida katika shughuli za wakulima kwa kufanya yafuatayo:-***

Matarajio ya 2020-2025 ni kusisitiza kilimo biashara katika uzalishaji ili kuongeza tija na faida kwa watendaji (*Actors*) wa tasnia za Kilimo ikiwemo matumizi ya teknolojia (miche bora, mbolea, zana, viwanda, maghala na vyumba baridi). Kwa

mfano katika misimu ya 2015-2020 wastani wa mahitaji pembejeo za kilimo yalikuwa tani **88,910** za mbolea, **Lita 1,232,277** za viuatilifu (vimiminika), tani **5,894** za viuatilifu vya yabisi na tani **72,176** za mbegu bora. Matarajio ya 2020- 2025 ni kufanya yafuatayo:

i. Kuhamasisha uzalishaji wa miche bora ya mazao ya kimkakati ya kibiashara
   - **a.** Kahawa kutoka miche **2,400,000** hadi **12,000,000.**
   - **b.** Korosho kutoka miche **499,284** hadi **1,656,000.**
   - c. Chai kutoka miche **507,000 (2018/19)** hadi **600,000.**
   - d. Kakao kutoka miche **25,000 (2019)** hadi miche mipya **100,000**.
   - e. Kwa zao la Michikichi kuna hatua za Utafiti zinaendelea Wilayani Kyela za kuzalisha mbegu mama.

ii. Kuongeza usambazaji na matumizi ya pembejeo za kilimo na kwa gharama nafuu.
   - **a.** Mbolea kutoka tani **88,910** hadi **115,583**
   - **b.** Mbegu bora kutoka tani **72,176** hadi **79,394**
   - c. Viuatilifu
     - ➢ Viuatilifu yabisi kutoka tani **5,894** hadi **6,483**
     - ➢ Viuatilifu vimiminika kutoka Lita **1,232,277** hadi **1,355,505**

iii. Kuhamasisha wadau kuanzisha kiwanda 1 cha mbolea.

iv. Kuboresha vituo 10 vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (*Ward Resource Centers*) kwa kuweka mifumo ya teknolojia za kisasa ili kuwezesha wadau wa SZK kupata taarifa mbalimbali kwa njia ya kieletroniki.

v. Kuongeza tija ya uzalishaji kwa mazao ya kipaumbele ya chakula ambayo ni mahindi, mpunga, maharage, ndizi na viazi mviringo. Wastani wa tija ya uzalishaji wa mazao ya kipaumbele ya chakula (2015 – 2020) na matarajio ya ongezeko la tija (2020 – 2025) umeainishwa katika Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na. 8**: Matarajio ya Tija kwa Mazao ya Kipaumbele ya Chakula

| Mazao | Wastani wa Tija (Tani/Hekta) | | Ongezeko (%) |
|---|---|---|---|
| | 2015 - 2020 | 2020 - 2025 | |
| Mahindi | 3.0 | 3.5 | 17.2 |
| Maharage | 1.5 | 2.5 | 63.0 |
| Mpunga | 4.6 | 6.0 | 30.5 |
| Ndizi | 14.1 | 16.0 | 13.9 |
| Viazi (Mv) | 20.2 | 25.0 | 23.6 |

**Chanzo:** Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri, 2020

vi. Kuongeza uzalishaji na tija kwa mazao ya kimkakati ya biashara ambayo ni Kahawa, Chai, Tumbaku, Pareto, Kakao, Michikichi na Korosho, Jedwali Na. 9 linaonesha matarajio ya tija kwa mazao haya kwa 2020 – 2025.

**Jedwali Na. 9:** Matarajio ya Tija na Ubora kwa Mazao ya Kimkakati ya Biashara

| MAZAO | TIJA (TANI/HEKTA) | | UBORA/DARAJA | |
|---|---|---|---|---|
| | 2015 - 2020 | 2020 - 2025 | 2015 - 2020 | 2020 - 2025 |
| Kahawa | 0.35 | 0.6 | 7 | 3 |
| Chai | 4.57 | 7 | - | - |
| Tumbaku | 1.39 | 1.5 | 75% | 85% |
| Pareto | 0.49 | 0.7 | 1.2 | 1.7 |
| Kakao | 1.30 | 1.5 | - | - |
| Michikichi | 1.29 | 2.0 | - | - |
| Korosho | 0.33 | 0.5 | - | - |

**Chanzo:** Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mbeya na Halmashauri, 2020

vii. Kuhamasisha wadau kuanzisha mashamba makubwa (*Block Farming*) ya Korosho matatu yenye ukubwa ekari **20,000** kila moja.
**viii.** Kuongeza wastani wa uzalishaji wa mazao ya mboga kutoka tani **156,718** hadi tani **172,390** na Matunda kutoka tani **990,663** hadi tani **1,089,729.**
ix. Kuhamasisha wadau kuwekeza kwenye ujenzi wa vyumba baridi (*Cold rooms*) kutoka **4** hadi **6**.
**x.** Kuongeza uzalishaji kutoka tani **23,671.6** hadi tani **31,562** na tija kutoka **1.5** hadi **2** kwa zao la alizeti.
xi. Kuongeza uzalishaji wa zao la michikichi kutoka tani **2,489** hadi **3,102** na tija kutoka **1.6** hadi **2** kwa mwaka.
**xii.** Kuongeza uzalishaji wa zao la Ngano kutoka tani **7,124** hadi **7,837.**


***C. Kuwezesha uwekezaji katika kilimo kwa kufanya yafuatayo:-***

i. Kuhamasisha wadau kujenga viwanda vya kusindika mazao kutoka viwanda **1,400** vilivyopo sasa hadi **1,540.**
ii. Kuhamasisha wadau kujenga maghala ya kuhifadhia mazao katika Halmashauri 7 za Mkoa.
**iii.** Kuhamasisha mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani katika maghala **10** mazao ya mpunga, mahindi, ufuta na korosho ifikapo 2025.

## 4.2 Sekta ya Mifugo 2015-2020 na Mpango Mkakati wa 2020-2025

### 4.2.1 Hali ya Uzalishaji wa Mifugo kwa kipindi cha 2015-2020

Sekta ya mifugo imeendelea kuwa sekta ya kipaumbele katika kuchochea maendeleo kwa wananchi wa Mkoa wa Mbeya. Sekta hii imekuwa ikitoa ajira, kuwezesha wananchi kujikwamua kiuchumi, kuzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda na kuchangia pato la Taifa. Mkoa wa Mbeya una jumla ya mifugo **3,304,315** kati yake ng'ombe ni **608,236** (509,767 asili na 98,469 kisasa), Mbuzi **195,569** (Asili 193,248 na Maziwa 2,321), Nguruwe **90,593**, kondoo ni **79,850,** kuku **2,035,080** (1,933,622 Kienyeji na 101,458 kisasa) na mifugo mingineyo **143,674.**




**Umbo Na. 1:** Idadi ya Mifugo

#### 4.2.2 Miundombinu na Malisho ya Mifugo

Mkoa una machinjio **33** na makaro **85** ambayo yamejengwa na kukarabatiwa kupitia programu ya ASDP na Mpango wa Kuendeleza Ngozi Tanzania. Aidha, Mkoa una majosho **99,** vituo **29** vya kutolea huduma za mifugo na maduka **720** ya kuuzia nyama. Katika kuepusha migororo ya wakulima na wafugaji, Mkoa kwa kupitia Halmashauri umeweza kutenga Hekta **1,343,155** kwa ajili ya malisho katika Halmashauri ya Chunya na Mbarali.

Vile vile, kuna shamba la kuzalisha mbegu za malisho la Wizara ya Mifugo na Uvuvi eneo la Langwila Wilayani Mbarali lenye ukubwa wa Hekta **294.** Shamba hilo huzalisha mbegu za malisho kwa ajili ya mashamba darasa kwa wafugaji na kwa matumizi ya taasisi na watu binafsi. Pia, kuna Kituo cha Utafiti wa Mifugo (TALIRI) – Uyole ambacho huzalisha na kusambaza mbegu aina ya Rhodes Boma, miti malisho na majani makavu (*Hay*) kwa ajili kituo na wafugaji.

#### 4.2.3 Magonjwa ya Mifugo ya Kimkakati

Serikali imeweka mkakati madhubuti wa kudhibiti magonjwa ya mifugo 13 ya kimkakati kana yanavyoonekana kwenye jedwali Na. 10. Aidha Serikali imezalisha chanjo ambazo zimeanza kuuzwa kwa bei elekezi kama ifuatavyo;

**Jedwali Na. 10:** Bei Elekezi ya Magonjwa 13 ya Mifugo ya Kimkakati

| Na | Aina ya Chanjo | Bei Elekezi (TZS) |
|---|---|---|

| | | Dukani/dozi | Kuchanja/ mfugo |
|---|---|---|---|
| 1 | Ugonjwa wa Homa aya Mapafu kwa ng'ombe (CBPP) | 300 | 550 |
| 2 | Ugonjwa wa chambavu (Black quarter) | 500 | 800 |
| 3 | Ugonjwa wa kimeta (Anthrax) | 250 | 500 |
| 4.a | Mchanganyiko wa Chambavu na Kimeta (TECOBLAX) kwa ng'ombe | 560 | 800 |
| 4.b | Mchanganyiko wa Chambavu na Kimeta (TECOBLAX) kwa mbuzi na kondoo | 280 | 500 |
| 5 | Ugonjwa wa kutupa mimba (Brucellosis) | 1,000 | 1,500 |
| 6 | Ugonjwa wa mdondo (New castle disease) | 50 | 50 |
| 7 | Ugonjwa wa Mapele ngozi (Lumpy skin disease) kwa ng'ombe | 400 | 600 |
| 8 | Ugonjwa wa sokota ya mbuzi na kondoo (Peste Petitis Rumanantes, (PPR) | 200 | 350 |
| 9 | Ugonjwa wa homa ya mapafu ya mbuzi (CCPP) | 200 | 350 |
| 10 | Ugonjwa wa miguu na midomo (FMD) | 2,500 | 3,000 |
| 11 | Ugonjwa wa kichaa cha mbwa (Rabies) | 1,000 | 1,500 |
| 12 | Ugonjwa wa Ndigana kali (ECF) | 10,000 | 17,000 |
| 13 | Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa (Fift valley fever, (RVF) | 400 | 700 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi, 2020

### 4.2.4 Mkakati wa Kuongeza Uzalishaji na Tija (2020-2025)

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo Mkoa unadhamiria kuleta mabadiliko makubwa katika ufugaji wa kisasa wenye kuzingatia kinga, tiba na utafiti wa mifugo ili kuongeza uzalishaji na tija kwa ajili ya ustawi wa wananchi. Mkazo mkubwa umewekwa kwa ufugaji unaozingatia watumiaji wengine wa ardhi kwa ajili ya kupunguza migogoro ambapo Mkoa umepanga kufanya yafuatayo:-

**A. *Kuendeleza na kuimarisha huduma za Ugani katika ngazi za Kata na Vijiji kwa kuhakikisha kuwa kila mfugaji anafikiwa na huduma za Ugani na kwa wakati kwa kutekeleza yafuatayo: -***

i. Kusimamia utoaji wa elimu ya ufugaji bora, umiliki wa ardhi na elimu ya mikopo kwa wafugaji **15,243** hadi **25,679**.
ii. Kusimamia uwezeshaji wa Vikundi vya wafugaji ili kupata dhamana kwenye taasisi za fedha kutoka **69** hadi vikundi **130**.
iii. Kusimamia mashamba darasa ya malisho ya mifugo ya asili ili wafugaji wajifunze jinsi ya kuboresha hifadhi ya malisho (*Feed Bank*) wakati wa ukame kutoka mashamba **48** hadi mashamba **96**.
iv. Kuhamasisha wafugaji kujiunga katika vikundi au vyama vya ushirika na kuwaunganisha na Taasisi za fedha kwa ajili ya kupatiwa mikopo kutoka vyama/vikundi **273** mpaka **362**.

v. Kusimamia mafunzo ya ufugaji bora katika vyama/vikundi vya wafugaji kutoka **273** hadi **362**.
vi. Kusimamia utoaji wa elimu ya matumzi ya teknolojia ya uhimilishaji kwa Wataalamu wa mifugo kutoka wataalam **14** hadi kufikia wataalam **50** ili kuboresha koosafu/mbari za mifugo.
vii. Kubuni na kutekeleza mipango ya kutoa mafunzo rejea mara **18** mpaka mara **70** kwa wafugaji na maafisa ugani katika Halmashauri zote za Mkoa kwa kushirikiana na sekta binafsi.

***B. Kuboresha afya ya mifugo nchini kwa kuimarisha kinga, chanjo na tiba kwa kufanya yafuatayo: -***

i. Kuhakikisha kuwa mifugo yote katika Halmashauri 7 inapatiwa chanjo kwa kuzingatia mpango na ratiba ya chanjo ya kitaifa.
ii. Kuhakikisha kuwa maeneo yote yenye majosho katika vijiji yanatambuliwa, yanapimwa na kupatiwa hatimiliki ambapo jumla ya maeneo yenye majosho 99 yatapimwa.
iii. Kusimamia chanjo mbalimbali za mifugo (ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na mbwa) kutoka mifugo **1,395,896** iliyochanjwa hadi **6,976,480**.
**iv.** Kusimamia matumizi ya dawa za ruzuku za kuogeshea mifugo kutoka lita **687.5** za dawa za ruzuku ya kuogeshea mifugo mpaka lita **4,826.5**.
v. Kuongeza uzalishaji wa mitamba kutoka **968** hadi mitamba **3,840** na kuisambaza kwa wafugaji kwa nia ya kuendelea kuzalisha mitamba ili kuhamasisha ufugaji wa kisasa.
vi. Kuongeza juhudi katika uhimilishaji ili kuongeza idadi ya ng’ombe wanaohimilishwa kutoka ng’ombe **6,000** mpaka ng’ombe **25,000**.
vii. Kuendelea kuimarisha utambuzi na usajili wa mifugo nchini ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wafugaji na mifugo yao kwa njia ya chapa na hereni za ng’ombe kutoka ng’ombe **471,418** mpaka **502,588**.
viii. Kuongeza idadi ya majosho kutoka 99 mpaka kufikia majosho 140 ili kupunguza vifo vya mifugo vitokanavyo na magonjwa ya kupe.
ix. Kuhakikisha kituo cha mfumo baridi (*Cold Chain*) kimoja cha Mkoa kina anzishwa na vituo 7 katika Halmashauri zote kwa ajili ya kutunza chanjo za mifugo.
x. Kusimamia maboresho ya kituo cha uchunguzi wa magonjwa ya mifugo cha Mkoa na kusimamia uanzishaji wa kliniki za huduma ya mifugo katika Halmashauri 7.

***C.* Kuimarisha huduma za maji, malisho na vyakula vya mifugo kwa kutekeleza yafuatayo: -**

i. Kuhamasisha/kusimamia ujenzi na ukarabati wa Miundombinu ya mifugo yaani malambo, majosho, machinjio, n.k kutoka Majosho **(99),** Machinjio **(16),** hadi

kufikia majosho **(140),** Machinjio **(33),** ili kuongeza idadi ya majosho katika wilaya zenye mifugo mingi hasa Chunya, Mbeya DC na Mbarali.

ii. Kuhamasisha na kusimamia upimaji na umilikishwaji kwa wafugaji maeneo ya malisho kutoka hekta **24,023** hadi kufikia hekta **268,631** ifikapo 2025 ili kuongeza maeneo ya ufugaji yaliyopimwa na yenye hati.

iii. Kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha viwanda vya maziwa na mazao mengine yatokanayo na mifugo kutoka viwanda vidogo **17** vya maziwa na kiwanda kikubwa kimoja (1) vilivyokuwa vimeanzishwa hadi hadi kufikia viwanda vidogo **22** na viwanda vikubwa **2**.

iv. Kuhamasisha na kuvutia wawekezaji kuwekeza kwenye viwanda viwili vya nyama.

v. Kuweka mkazo zaidi kwenye usambazaji wa teknolojia na kutoa mafunzo kwa wafugaji na wadau wote kwa njia ya machapisho, majarida, vipeperushi, vipindi vya redio kutoka machapisho 3,500 na vipindi vya redio vitatu mpaka machapisho 7,000 na vipindi 20 vya redio.

vi. Kuongeza malambo na mabwawa ya maji ya mifugo kwa kukarabati na kujenga mabwawa mapya kutoka mabwawa 7 yaliyopo hadi 16 na visima 12 hadi 17.

## 4.3 Sekta ya Uvuvi 2015-2020 na Mpango Mkakati wa 2020-2025

### 4.3.1 Hali ya Uzalishaji wa Sekta ya Uvuvi (2015-2020)

Sekta ya Uvuvi ni moja kati ya sekta muhimu za kiuchumi katika Mkoa. Shughuli za uvuvi zinahusisha uvuvi kwenye maji ya asili na ukuzaji viumbe majini. Mwaka 2015 Sekta ya Uvuvi imekuwa ikichangia asilimia **1.09** kwenye Pato la Mkoa na ina kua kwa asilimia **1** (NBS, 2015**).** Aidha, Sekta hiyo huchangia katika uhakika wa chakula, lishe, kuongeza kipato, fedha za kigeni na kupunguza umaskini. Inakadiriwa kuwa zaidi ya Wananchi **100,000** wanategemea shughuli zinazohusiana na uvuvi.

Shughuli za uvuvi kwenye Mkoa wetu zinafanyika kwenye Ziwa Nyasa, Mabwawa ya asili, mito na mabwawa ya kuchimbwa. Mkoa una jumla ya mabwawa ya kuchimbwa **1,744** ambayo kwa wastani yanazalisha samaki tani **72.4** kwa mwaka. Uwepo wa Ziwa Nyasa na mito ya asili vimechangia kwa kiasi kikubwa uvunaji wa samaki kwa mwaka wastani wa samaki tani **18,546.01** hupatikana kupitia vyanzo hivi. Katika kipindi hiki hakuna uwekezaji uliofanyika wa ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba (*Cage Culture*) kwenye Ziwa Nyasa fursa ambayo inaweza kutumika kuongeza uvunaji wa samaki. Kuwepo kwa aina zaidi ya **400** za samaki wa mapambo kunaweza pia kutumika kama fursa ya kuvutia wawekezaji kwenye eneo hilo. Pamoja na fursa hii ya uwepo wa ziwa, mabwawa na mito ya asili bado Mkoa unakabiliwa na changamoto ya uvuvi haramu jambo ambalo linaathiri samaki, mazalia yao na afya ya mlaji.

### 4.3.2 Mkakati wa Kuongeza Uzalishaji na Tija (2020-2025)

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Mkoa utahakikisha sekta ya uvuvi inaimarika kwa kuongeza matumizi ya sayansi na teknolojia ya uvuvi endelevu ili kuwa shindani na yenye kuchangia kwa kiasi kikubwa usalama wa chakula na kipato. Ili kufanikisha haya Mkoa umepanga kufanya mambo yafuatayo:-

i. Kuongeza idadi ya doria kwenye Ziwa Nyasa, mito na mabwawa ya asili kutoka 241 hadi 350 ili kupambana na uvuvi haramu na kuifanya sekta iwe endelevu na yenye tija.
ii. Kuboresha Mialo ya kupokelea samaki **12** iliyopo sasa na kujenga Mialo mingine mipya **12** kwenye Ziwa Nyasa.
iii. Kusimamia na kuongeza vikundi vya kusimamia rasilimali za uvuvi (*BMUs*) katika Ziwa Nyasa. Mkoa una vikundi **12** na unatarajia kuongeza vikundi vipya **12** kwa miaka mitano ijayo.
iv. Kuhamasisha ufugaji wa Samaki kwa kuongeza idadi ya mabwawa kutoka **1,744** hadi **3,744**.
v. Kutoa elimu ya uvuvi endelevu kwa Wavuvi **1,471** (Kyela 1,326 na Mbarali 145).
vi. Kutoa mafunzo ya ufugaji bora wa samaki kutoka wafugaji **1,230** hadi **2,730**.
vii. Kuhamasisha wadau kuanzisha kituo **1** cha kuzalisha na kukuza viumbe majini (*Aquaculture*).
viii. Kuhamasisha wadau kuwekeza kwenye ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba (*Cage Culture*) kwenye Ziwa Nyasa.
ix. Kuhamasisha wadau kuwekeza kwenye fursa ya biashara ya samaki wa mapambo kwenye Ziwa Nyasa

## 4.4 Sekta ya Ushirika

### 4.4.1 Hali ya Ushirika katika Mkoa

Hadi kufikia Mwezi Juni 2020, Mkoa ulikuwa na jumla ya vyama hai vya ushirika **464 vyenye** jumla ya wanachama **84,239** baada ya vyama vya ushirika **68** kufutwa kwenye daftari la Vyama vya ushirika. Kwa sasa Mkoa una Vyama Vikuu vya Mazao **4,** Chama Kikuu kimoja **(1)** cha Maziwa na chama kimoja **(1)** cha Mradi wa Pamoja wa wakulima wa chai. Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) ni **169,** vyama vya mazao **185,** Ufugaji **51,** Umwagiliaji **15** Uvuvi **19,** pia kuna vyama vingine vya huduma **18.** Jedwali Na. 11 linaonesha idadi ya vyama vya Ushirika.

**Jedwali Na. 11:** Idadi ya Vyama Vikuu / miradi wa Pamoja, SACCOS, na Vyama Vingine vya Ushirika

| Halmashauri | Vyama Vikuu/ Mradi | SACCOS | AMCOS | Wafugaji | Wavuvi | Umwagiliaji | Vyama Vingine | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Busokelo | 0 | 4 | 31 | 12 | 0 | 0 | 0 | 46 |
| Chunya | 1 | 8 | 23 | 2 | 2 | 0 | 0 | 36 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kyela | 1 | 7 | 39 | 1 | 3 | 0 | 0 | 52 |
| Mbarali | 0 | 25 | 9 | 4 | 4 | 11 | 4 | 57 |
| Mbeya-J | 1 | 69 | 1 | 4 | 5 | 4 | 12 | 95 |
| Mbeya-DC | 0 | 26 | 34 | 2 | 2 | 0 | 2 | 65 |
| Rungwe | 3 | 31 | 48 | 26 | 3 | 0 | 0 | 111 |
| **JUMLA** | **6** | **170** | **185** | **51** | **19** | **15** | **18** | **464** |

**Chanzo:** Ofisi ya Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mbeya, 2020

Kazi kubwa iliyofanyika katika vyama hivi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ni pamoja na uhamasishaji, uanzishaji wa vyama vipya na uimarishaji wa vyama hivyo, uchaguzi wa viongozi kulingana na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na 6 ya Mwaka 2013, uboreshaji Daftari la Vyama vya Ushirika, Ukaguzi na Mafunzo kwa viongozi, watendaji na wanachama.

### 4.4.2 Huduma za Vyama vya Ushirika

#### A. Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS)

Idadi ya *SACCOS* ni 170 zenye jumla ya wanachama **45,134** na mtaji wa shilingi **82,004,765,299.00.** Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita *SACCOS* zimetoa mikopo wa jumla ya shilingi **64,491,741,759** kwa wanachama. Mbali na kuwanufaisha wanachama kwa kuwapa mikopo, *SACCOS* zimeweza kutoa ajira kwa watu 306, kutoa misaada katika jamii na kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wanachama.

#### B. Vyama vya Ushirika vya Mazao (*AMCOS*)

Vyama vya ushirika vya msingi vya mazao vipo 185 vyenye jumla ya wanachama 33,606. Vyama hivi vipo kwenye mazao yafuatayo:

**Tumbaku**

Tumbaku inazalishwa katika Wilaya ya Chunya, Wilaya ina jumla ya Vyama vya Ushirika 19 vinavyojishughulisha na zao hilo. Uzalishaji kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, vyama hivi vimeweza kuuza tumbaku jumla ya **Kilogramu 46,788,942.7** zenye thamani ya **Tsh. Bilioni 175,100,387,916.10.**

**Kahawa**

Kahawa inazalishwa katika Wilaya za Rungwe na Mbeya. Kuna jumla ya Vyama vya Ushirika 70 vinavyojishughulisha na zao hilo. Uzalishaji kwa kipindi cha Mwaka 2018/2019 na 2019/2020, Vyama hivi vimeuza jumla ya **Kilogramu 5,308,036** zenye thamani ya **Tsh. 17,415,666,116/=**.

**Kokoa**

Mkoa umeendelea kutekeleza mfumo wa stakabadhi ghalani kwa zao la kakao. Mfumo huu ulianza kutekelezwa Mwezi Oktoba, 2018 katika Halmashauri za Rungwe, Busokelo na Kyela. Kakao yote ya Wakulima imekuwa ikiuzwa kupitia

utaratibu wa minada. Jumla ya minada 75 imefanyika na **Kilogramu 14,387,323.53** zimeuzwa tangu kuanza kwa mfumo huu hadi kufikia tarehe 19 Juni 2020 na wakulima wamelipwa Jumla **Tsh. 68,470,229,511**/=. Kakao imeuzwa kwa bei kati ya **Tsh. 3,700-5,787/=** katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2018 hadi Juni 2020.

**Chai**

Chai inazalishwa katika Wilaya ya Rungwe, Wilaya ina jumla ya Vyama vya Ushirika vya Msingi 9 vinavyojishughulisha na zao la chai. Msimu wa mwaka 2019/2020 jumla ya kilo **13,376,295.8** zimeuzwa kwa thamani ya **Tsh. 4,215,503,427/=**.

**C. Vyama Vingine vya Ushirika**

Mkoa una Vyama vingine vya shughuli mbalimbali 103 vyenye jumla ya wanachama 5,499, vyama hivi vinatoa huduma katika nyanja za uvuvi, ufugaji, viwanda, usafiri, biashara, umwagiliaji na ubebaji mizigo.

### 4.4.3 Mafanikio ya Sekta ya Ushirika kwa Miaka Mitano (2015-2020)

i. Usajili wa Vyama vya Ushirika; Mwaka 2015 Mkoa ulikuwa na jumla ya Vyama vya Ushirika 406 hadi kufikia mwaka 2020 Mkoa una jumla ya Vyama vya Ushirika 464.

**ii.** Mtaji wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*); kwa mwaka 2015 mtaji umeongezeka kutoka**Tsh. Bilioni 16,584,185,546** na umefikia kiasi cha **Tsh. Bilioni 82,004,765,299/=**

**iii.** Mikopo iliyotolewa kupitia Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) kwa kipindi cha miaka mitano ni jumla ya **Tsh. Bilioni 64,491,741,759/=**

iv. Mkoa umefanikiwa kuboresha mfumo wa mauzo ya mazao ya wakulima kupitia Vyama vya Ushirika kwa mazao ya Kimkakati ya Biashara (Kahawa, Tumbaku, Chai na Korosho)

v. Kuanzisha Mfumo wa Stakabadhi Mazao Ghalani kwa zao la Kakao

   a. Mkoa umefanikiwa kuanzisha mfumo wa Stakabadhi Ghalani kwa zao la kakao kupitia vyama vya Ushirika na kuboresha Minada ya Kakao inayokutanisha wakulima na wanunuzi

   **b.** Bei ya kakao kwa wakulima wa Kakao imepanda kutoka **Tsh. 2,800** mwaka 2015 hadi **Tsh. 5,030** mwaka 2020

vi. Ajira kwenye Vyama vya Ushirika; Kufikia mwaka 2020 Vyama vya Ushirika vimetoa jumla ya ajira kwa watumishi 307 kutoka watumishi 107 mwaka 2015.

**vii.** Vyama vya Ushirika vimefanikiwa kupata faida na kutoa Gawio la faida kwa wanachama wake kiasi cha **Tsh. 755,659,536/=**

viii. Vyama vya Ushirika **19** vimefanikiwa kuagiza Pembejeo kwa pamoja kupitia mfumo wa ununuzi wa pamoja (*BPS*) na mifumo mingine kuhakikisha wanachama wanapata Pembejeo kwa wakati na zenye ubora.

### 4.5 Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Ushirika 2020-2025

i. Kuhakikisha Vyama Vikuu 5 vya Ushirika na Mradi wa Pamoja, vinasimamia na kuhudumia Vyama vyake vya Msingi, kwa kusimamia uzalishaji, upatikanaji wa masoko, upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani na kuajiri watendaji wenye sifa.

ii. Kuimarisha uendeshaji wa mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani kwa maghala 5.

iii. Kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuanzisha na kumiliki Viwanda ili kuongeza mnyororo wa thamani kwenye mazao ya kilimo na ufugaji kutoka Viwanda 19 hadi 30

iv. Kuhamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika vinavyogusa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii kutoka Vyama vya Ushirika 463 kufikia vyama 520

v. Kuhamasisha na kusimamia Vyama vya Ushirika kuongeza mitaji kwa Vyama 520.

vi. Kuratibu na kusimamia Elimu na Mafunzo ya Ushirika kwa Wanachama, viongozi, na watendaji wa Vyama **520** vya ushirika na wadau mbalimbali.

vii. Kuhamasisha wananchi kujiunga na Vyama vya Ushirika ili kuongeza idadi ya wanachama kutoka **119,980** kufikia **300,000**.

viii. Kuimarisha utawala bora kwa kuboresha uongozi, kudhibiti wizi na ubadhirifu ndani ya Vyama vya Ushirika.

ix. Kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa mara kwa mara kwa vyama 520 vya Ushirika.

# SURA YA TANO
# UFUATILIAJI NA TATHMINI

## 5.0 Utangulizi

Lengo ni kufuatilia na kupima matokeo ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Sekta za Kilimo kwa kila mwaka.

## 5.1. Ufuatiliaji

Ufuatiliaji utafanyika kwa kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa na takwimu za mafanikio ya mpango mkakati kuelekea malengo yaliyokusudiwa. Sambamba na Malengo ya Programu ya *ASDP* II, Mipango na Bajeti za kuendeleza Mpango wa Maendeleo ya Kilimo Ngazi ya Wilaya (*DADPs*), na wadau wengine wa Maendeleo waliopo kwenye Halmashauri. Ufuatiliaji utafanyika kwa kuhimiza utekelezaji wa Ubia baina ya Sekta Binafsi na ya Umma (*Public Private Partnership*).

## 5.2. Tathmini

Tathmini itafanyika kwa kuzingatia kikamilifu malengo na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa SZK. Kazi hii itafanyika mara mbili kwa mwaka ili kuweza kuboresha/kurekebisha malengo kutokana na mwenendo wa matokeo yatakayokuwa yanafikiwa kwa kila shabaha iliyopangwa. Hivyo, ni muhimu kwa kila Halmashauri kuweka shabaha zinazoakisi malengo ya Mpango Mkakati wa kuendeleza Sekta za Kilimo 2020-2025.

## SURA YA SITA
## HITIMISHO

Mkoa unaamini kuwa changamoto nyingi zilizopo katika Sekta za Kilimo (Kilimo, Mifugo na Uvuvi) zitapungua endapo tutatekeleza Kilimo Biashara kwa kuboresha matumizi ya teknolojia katika kuongeza tija, ubora na upatikanaji wa masoko ya mazao. Hali hii itawezesha kuongeza kipato, ajira na mali ghafi kwa ajili ya viwanda.

Kwa mantiki hii mkakati huu umejikita zaidi katika kuimarisha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (*PPP*) kama namna bora ya kushughulikia changamoto za kifedha, usimamizi na kuimarisha huduma za sekta za kilimo.

Kwa kuhitimisha, katika kufanikisha utekelezaji wa Mkakati huu, majukumu na kazi za msingi za Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni kama ifuatavyo;

- ✓ Sekretarieti ya Mkoa itaendelea kujenga uwezo, kuratibu na kufuatilia utekelezaji katika ngazi ya Halmashauri, sambamba na kuwa kiungo kati ya Wizara za Kisekta.
- ✓ Halmashauri itaendelea kuratibu, kusimamia na kufuatilia shughuli zote za utekelezaji wa maendeleo ya sekta za kilimo. Kazi hii itafanyika kwa kushirikiana na sekta binafsi, wakiwemo wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanya biashara, wasindikaji, wadau wa maendeleo, na vyama vya ushirika katika kufanya yafuatayo;
    - ❖ Kuhimiza utashi wa Viongozi wa ngazi zote kuwekeza katika sekta za kilimo;
    - ❖ Kuandaa mpango kazi wa utekelezaji wa Mkakati wa Sekta za Kilimo (2020 – 2025);
    - ❖ Kuhimiza utekelezaji wa mfumo thabiti wa kuimarisha uwekezaji katika sekta za kilimo sambamba na mahitaji ya soko; na;
    - ❖ Kusimamia na kuhakikisha kuwa watendaji wa kisekta, katika ngazi zote za Wilaya, wanatimiza wajibu wao.
- ✓ Sekta binafsi kushirikiana na sekta ya Umma katika kuongeza uwezo na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu mbalimbali. Hii ni pamoja na kufikisha huduma za kiuchumi na kijamii, na upatikanaji wa huduma bora.